## Suala kuu la 10

## Heshimu imani yangu

*Jianna aliporejea nyumbani kutoka shuleni jioni hiyo, alimwendea baba yake kwa unyenyekevu. Alimwomba amruhusu kuitumia kompyuta yake, kutafuta habari kuhusu dini mbalimbali ili ajisomee.*

*“Uko radhi, binti yangu. Nilivyokushauri awali, sharti uzingatie hatua zote za kiusalama. Sawa?” Baba alimkumbusha naye binti akatii.*

*Jianna alichapisha mada, ‘visa kuhusu dini’, akaona kimoja chenye anwani: ‘HESHIMU IMANI YANGU’. Moja kwa moja, alianza kukisoma.*

“Leo kelele zenu hazikufua dafu. Tumeimba hadi pambio zikaisha. Natumai mmeburudika,” David alimchokoza Neema.

“Heshimu imani yangu, David. Hilo si jambo la kufanyia mzaha,” alisema Neema akiwa amepandwa na hasira.

Neema alifululiza hadi kwa mwalimu mkuu kwenda kumshtaki David kwa kumkosea. Alimweleza mwalimu mambo yote ambayo David alikuwa amesema. Mwalimu mkuu alimwambia akamwite David.

David alipofika ofisini kwa mwalimu mkuu, yeye pia alitoa malalamishi yake. Ikawa kwamba wote walidai imani zao hazikuheshimiwa. Walisema kuwa kipindi kilichokuwa kimetengwa kwa ajili ya sala za waumini tofauti shuleni, kilikuwa kimegeuka mashindano. Kila kundi lilijaribu kuonyesha kuwa lilikuwa bora kuliko jingine kwa jinsi walivyofanya mambo yao.

“Neema na David, ni muhimu kuheshimu imani ya kila mmoja. Kipindi hiki kilichotengwa cha sala hakifai kuwa cha kuwatenganisha, bali cha kuwaunganisha kwa kuonyesha kuwa tunaheshimu imani zetu, japo ni tofauti,” mwalimu mkuu alifafanua.

Mwalimu mkuu aliwashauri waridhiane na kuichukulia imani ya kila mmoja kuwa na umuhimu, jinsi yao ilivyo. Baada ya hayo, aliwaagiza warudi darasani.

Mwalimu mkuu alibaki akiwaza na kuwazua. Jioni ile, aliwaita walimu wote ili kulijadili suala lile. Walimu wote waliamua kwa kauli moja kuwa watakuwa na siku moja ya sala ya pamoja ambayo itashirikisha wanafunzi na walimu wote shuleni, bila kujali tofauti zao za kiimani.

"Hiyo ndiyo njia pekee ya kumwezesha kila mwanafunzi kumthamini mwenzake na kuiheshimu imani ya mwenzake," mwalimu mkuu alisema.